**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS -TAMISEMI**

**MKOA WA DODOMA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**

**Shule ya sekondari msakwalo**
**S.L.P 362**
**CHEMBA**
**22/04/2024**

Kumb. Na. MSS/ADMN/FV 2024/2025
Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MSAKWALO MWAKA 2024**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule ya Sekondari **MSAKWALO** mwaka wa masomo **2024/2025** tahasusi ya……………..,Muhula wa masomo kwa kidato cha tano 2024 utaanza tarehe.................. Hivyo mwanzafunzi anatakiwa kuripoti tarehe ............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe..................

Shule ya Sekondari **MSAKWALO** inaanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, Kidato cha kwanza hadi cha nne ni shule ya kutwa mchanganyiko (wavulana na wasichana) na Kidato cha tano na sita ni shule ya Bweni wavulana tu. Ina michepuo minne (4) HGL, HGK, HGFa na HGLi.

Shule ipo wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, ipo umbali wa kilometa 164 Kaskazini mwa **Jiji la Dodoma.** Ukifika stendi Kuu ya Dodoma **(STENDI YA NANENANE)** panda daradara kwenda **stendi ya daladala (MACHINGA COMPLEX),** ukifika hapo utapata daladala za kukupeleka stendi ya **Chang'ombe juu,** ukifika huko uliza **mabasi ya usandawe (Ovada),** nauli ni **Tsh 11,000/=** hadi kufika Msakwalo Sekondari. Kwa atakayetokea **Singida** nauli ni **Tsh 10,000/=**

***RATIBA YA MAGARI.***

- Kwa Singida-OVADA (Msakwalo) magari yapo kila siku mchana.
- Kwa Dodoma-OVADA (Msakwalo) magari yapo kila siku isipokuwa siku ya **IJUMAA** na yanaondoka Dodoma saa nne kamili asubuhi (10:00am). Hivyo unashauriwa kufika Dodoma siku moja kabla ya safari na ukate tiketi yako mapema.

Wale wanaotoka Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa na Mkoa wa Kigoma washukie Mkoani Singida na waulizie magari ya kuelekea USANDAWE KWAMTORO AU OVADA (Msakwalo). Shule ipo mpakani mwa mkoa wa singida. **Jengo la utawala lipo umbali wa mita 200 kutoka Kibao cha shule**.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**Sare Za Shule.**

- Suruali mbili rangi ya dark blue wakati wa masomo, zisizobana (siyo modo) na ziwe na turn up.
- Shati mbili nyeupe za mikono mirefu zenye alama ya V kwenye bega mkono wa kushoto
- Tai ya dark blue, ni sehemu ya sare ya shule (uniform) ukiwa darasani
- Suruari 2 nyeusi kwa ajili ya shamba dress (itumike baada ya vipindi vya darasani tu).
- T-shirt 1 rangi ya bluu (bluu ya kawaida) kwa ajili ya shamba dress, iwe mpya kwa ajili ya kuweka nembo ya shule.
- Track suti moja rangi nyekundu.
- Sweta 1 rangi ya dark blue.
- Viatu vyeusi jozi 2 vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi wakati wa masomo.
- Soksi nyeupe jozi 2 wakati wa masomo na jozi mbili kijivu wakati wa michezo.
- Viatu aina ya raba, jozi 1 kwa ajili ya michezo.
- Kandambili za kuogea, **(Zitumike Bwenini Tu)**
- Sale za michezo, Bukta na t-shirt, rangi **nyekundu** kwa **HGK** na HGK ,**blue** kwa HGFa na HGLi **(zisiwe na maandishi yoyote au nembo ya timu yoyote ya mpira)**

**Michango Ya Shule.**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule nambari **A/C 50201200102** (NMB), jina la akaunti: **KDC MSAKWALO SECONDARY SCHOOL,** Katika benki ya **NMB au kwa wakala yeyote wa NMB.**

**NB**:Tafadhali **andika Jina la Mwanafunzi na sio jina la mzazi kwenye pay in slip ambayo ataiwasilisha shuleni**.

**MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI**:

i. Ream ya karatasi isiyo na mistari A4 bunda mbili **(02)** kwa mwaka.
ii. Bima ya afya, (ni mhimu sana mwanafunzi kuja na bima ya afya)P.
iii. Madaftari 12 ya"counter book quire 4"
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi kulingana na mchepuo wake tunashauri viwe vya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE),
v. Kamusi ya Kiswahili kwa **HGK na HGFa** na Advanced Dictionary kwa **HGL na HGLi** (vinakaguliwa katika ofisi ya taaluma).
vi. Scientific Calculator ( non programmable).
vii. Godoro lenye urefu wa futi **6**, upana futi **2½** (futi mbili na nusu) na unene wa inchi nne

viii. Mashuka jozi (pair) **2** rangi ya blue. **Blanket 1 (kuna baridi)**, Chandarua 1 rangi nyuepe.

ix. Nguo za ndani za kutosha;

x. Vyombo vya chakula (sahani ya mfupa, bakuli ya mfupa, kijiko na kikombe cha mfupa) **Vyombo vya plastic haviruhusiwi.**

xi. Ndoo mbili ndogo (lita10) zenye mifuniko.

xii. Reki 1 kwa HGK na HGK, panga 1 kwa HGFa na HGLi na Jembe 1 lenye mpini kwa wote.

xiii. Ufagio wa ndani 1 (soft bloom), Ufagio wa nje wa chelewa 1 na mopper 1 na hard bloom moja.

xiv. Dawa ya chooni lita 5 kwa wanafunzi wote

**MHIMU**:

**Siku ya kuripoti Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule. Asije na nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni.**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na asubuhi (night Preparation and Morning Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro,
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo,
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla,
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule,
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu; hairusiwi kufuga ndevu kata ndevu zako
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa
xi. Kusababisha mimba au kusababisha kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**HALBERTO VITUS KALIWABU.**
**MKUU WA SHULE**
**0737637654/0629140015**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MSAKWALO
S.L.P. 362 CHEMBA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ***Makamu Mkuu wa Shule 0735084260 (Mwl.Ahmed Ally Omary)***
- ***Mwandamizi Taaluma 0737961247 (Mwl. Erick Jeremiah Misangia)***
- ***Mwandamizi Malezi 0737665378 ( Mwl. Gabriel Pius Hinna)***
- ***Mwalim wa Fedha 0625327211 ( Mwl. Nicholaus Samson Tummah***

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**CHEMBA DISTRICT COUNCIL**
**MSAKWALO SECONDARY SCHOOL**

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by Medical Officer in respect of all Form V entrants)

Pupil's full name: ……………………………………………………………………

Age: …………… Years. Sex: ……….

Blood count (Red and White): ………………………………………………….

Stool Examination: ……………………………………………………………

Syphilis and other venereal diseases test: ……………………………………………..

T.B Test: ………………………………………………

Eye Test: ………………………………………………

Ears Test: ………………………………………………

Spleen: ………………………………………………

Abdomen: ………………………………………………

ADDITONAL INFORMATION

(If any) e.g. physical defects impairment, Infections, chronic or family diseases etc: ……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I certify that the above pupil is fit to pursue studies at MSAKWALO Secondary School.

Station ………………………………………….. Signature ………………………….

Date………………………………………… Designation ………………………………

NB: This form should be completed and submit to school on arrival.

**Fomu Na. 1**

**AHADI YA MZAZI / MLEZI**

Mimi______________________wa S.L.P______Mji__________Simu _____________ na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni ______________natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ___________________. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari MSAKWALO kuanzia tarehe _________________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina:_________________________ saini________________

Tarehe:_____________ Uhusiano na mwanafunzi:____________

**Fomu Na. 2**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi ________________________________Wa kidato cha Tano chaguo______________(tahasusi) mwaka wa masomo 2023/2024. Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari MSAKWALO. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:_________________________saini________________

Tarehe:_____________

**Fomu Na. 3**

**KIAPO CHA MZAZI / MLEZI**

Mimi:____________________wa S.L.P__________Mji__________ Simu Na____________ Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

| Picha ya ndugu wa kwanza |
|---|

Jina:____________________________ Kazi:____________ Makazi: _________________ Simu: ____________________

Uhusiano na mwanafunzi:____________________________________

| Picha ya ndugu wa Pili |
|---|

Jina:____________________________________________ Kazi:________

Makazi: ________________ Simu: ____________

Uhusiano na mwanafunzi:________________________________________

| Picha ya ndugu wa Tatu |
|---|

Jina:____________________________ Kazi:____________ Makazi: _________________ Simu: ____________________

Uhusiano na mwanafunzi:__________________________________